JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI NOVEMBA NA DESEMBA, 2024

### 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Novemba na Desemba, 2024 vipindi vya mvua vilijitokeza katika maeneo mbalimbali nchini, huku ongezeko kidogo la mvua likijitokeza mwezi Desemba. Hali hii ilisababisha ongezeko kidogo la unyevu ardhini, kina cha maji na malisho katika baadhi ya maeneo, lakini pia ilipelekea mafuriko na kutuama kwa maji katika baadhi ya maeneo. Hali ya joto inayoathiri shughuli zinazofanyika nje hasa nyakati za mchana ilijitokeza hususan katika maeneo yaliyopata vipindi vichache vya mvua. Aidha, vipindi vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kusini magharibi. Hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa mvua za Msimu (Vuli, 2024 na Msimu 2024/2025) zilizotolewa awali.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Novemba, 2024

Katika kipindi cha mwezi Novemba 2024, vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ukanda wa ziwa Victoria, pwani ya kaskazini, magharibi na kati mwa nchi. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika maeneo machache na kusababisha mafuriko, upotevu wa maisha, uharibifu wa mali na kuathiri shughuli za kiuchumi. Kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 91.7 kilirekodiwa katika kituo cha Handeni (mkoa wa Tanga) mnamo tarehe 30 Novemba, 2024 ikifuatiwa na milimita 77.0 katika kituo cha Mwanza mnamo tarehe 20 Novemba na milimita 73.7 katika kituo cha Ukiriguru (Mkoa wa Mwanza) mnamo tarehe 27 Novemba, 2024. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 1.


Ripoti kutoka katika vyombo vya habari zilithibitisha athari za mvua katika mwezi Novemba. Mnamo usiku wa tarehe 25 Novemba 2024, mvua zilizokuwa zikiendelea kunyesha na kupelekea kutokea mafuriko kutokana na kujaa kwa mto Mori uliopo wilaya ya Tarime, mkoa wa Mara zilisababisha watu tisa wa familia moja kufariki baada ya nyumba yao kusombwa na maji. Aidha, baadhi ya mali ikiwemo mashamba yaliathirika na hivyo kusabibisha adha kwa wakazi wa maeneo hayo. (*Chanzo. Gazeti la Mwananchi)*

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*




**Kielelezo 1:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Novemba, 2024

### 1.2 Hali joto kwa mwezi Novemba, 2024

Katika kipindi cha mwezi Novemba, 2024 hakuna vipindi vya baridi kali vilivyojitokeza nchini. Aidha, kiwango kidogo zaidi cha joto la chini cha nyuzi joto 11.4 °C Kilirekodiwa katika kituo cha Igeri (Mkoa wa Njombe) mnamo tarehe 3 Novemba, 2024.


Kwa upande wa viwango vya juu vya joto, hali ya joto zaidi ilijitokeza katika baadhi ya maeneo hususan maeneo ya ukanda wa pwani. Hali hii iliathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika maeneo ya wazi. Viwango vya juu vya joto vilirekodiwa katika mkoa wa Morogogo huku kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 38.4 °C ikifuatiwa na nyuzi joto 37.2 °C vikirekodiwa katika kituo cha Ilonga na Morogoro mtawalia mnamo tarehe 29 Novemba, 2024. Aidha, vituo hivi viliripoti viwango vya juu vya joto vinavyozidi nyuzi joto 35 °C kwa takribani siku 6 hadi 7 katika mwezi.

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Novemba, 2024

Katika mwezi huu, vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchiniikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba) na nyanda za juu kusini magharibi (Songwe). Kasi na nguvu ya upepo ilisababisha athari mbalimbali ikiwemo ongezeko la vumbi, kupeperusha takataka na kusabisha kupungua kwa uono. Maeneo ya mwambao wa pwani yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa ya bahari na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika mwambao.

### 1.4 Mvua kubwa kwa mwezi Desemba, 2024

Katika kipindi cha mwezi Desemba, 2024 vipindi vya mvua zilizoambana na ngurumo za radi vilijitokeza katika maeneo mengi nchini. Maeneo mengi yalipata mvua za wastani hadi juu ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu kwa mwezi Desemba. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo na kusababisha mafuriko, uharibifu wa maundombinu na mali, na kuathiri baadhi ya shughuli za kiuchuni wakati na baada ya matukio ya mvua kubwa. Kiwango cha juu zaidi cha mvua, milimita 91.8, kiliripotiwa katika kituo cha Lyamungu (mkoa wa Kilimanjaro) mnamo tarehe 2 Desemba, 2024 kikifuatiwa na milimita 90.3 katika kituo cha Songea (Mkoa wa Ruvuma) mnamo tarehe 3 Desemba na militima 76.2 katika kituo cha Ilonga (Mkoa wa Morogoro) mnamo tarehe 31 Desemba, 2024. Vituo vilivyoripoti vipindi vya mvua kubwa vya milimita 50 au zaidi ni kama vinavyoonekana kwenye Kielelezo 2.




**Kielelezo 2:** Viwango vya mvua kubwa kwa mwezi Desemba, 2024

### 1.5 Hali joto kwa mwezi Desemba, 2024

Katika kipindi cha mwezi Desemba 2024, vipindi vichache vya baridi vilijitokeza kwa nyakati za usiku hususan katika mikoa ya Mbeya na Njombe. Kiwango cha chini zaidi cha nyuzi joto 11.4°C kiliripotiwa katika kituo cha Uyole (Mkoa wa Mbeya) mnamo tarehe 13 na 14 Desemba, 2024. Kwa upande mwingine, baadhi ya maeneo hususan

ukanda wa pwani yalipata vipindi vya joto nyakati za mchana. Kiwango cha juu zaidi cha nyuzi joto 34.1 °C kilirekodiwa katika kituo cha Morogoro mnamo tarehe 14 Desemba, 2024.

**1.6 Upepo Mkali kwa mwezi Desemba, 2024**

Vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba) na nyanda za juu kusini magharibi (Songwe). Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo.

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 16 Januari, 2025*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**